

## **UTARATIBU WA KUPATA KIBALI CHA Kuingiza CHAKULA CHA SAMAKI NDANI YA NCHI**

### **A. Wadau wanaoweza kuingiza chakula cha samaki kutoka nje ya nchi**

- i. Serikali
- ii. Sekta binafsi (wafanyabiashara/Watengenezaji)
- iii. Wamiliki wa viwanda vya chakula cha samaki
- iv. Wafugaji wa samaki

### **B. Mambo ya kuzingatia wakati wa kuagiza chakula cha samaki kutoka nchi za nje**

- i. Wafugaji wa samaki:
  - a) Kibali cha kuanzisha shughuli za ukuzaji viumbe maji kibiashara.
  - b) Barua ya kuomba kibali cha kuingiza chakula cha samaki
  - c) Nyaraka ya manunuzi kutoka kwa muuzaji “proforma invoice”
  - d) Ripoti ya uchunguzi wa ubora wa chakula cha samaki kutoka kiwandani “Feed Analysis Report”
  - e) Cheti cha ubora “Sanitary/health Certificate” kutoka kiwandani
  - f) Cheti cha mlipa kodi (endapo msamaha wa kodi utahitajika)
  - g) Barua ya kuomba msamaha wa kodi

### **Angalizo:**

- ✓ Maombi yote yaliombatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu yanatumwa kupitia anuani ya Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Uvuvi.
- ✓ Kwa maombi yaliyokamilika, yataendelea na taratibu na kupewa kibali.

### **C. Mambo ya kuzingatia baada ya kupata kibali cha kuagiza chakula cha samaki kutoka nchi za nje**

Chakula cha samaki kitakapowasili bandarini /mpakani, kitakaguliwa na maafisa wa mamlaka tofauti kabla hakijaruhusiwa kutoka kwa ajili ya matumizi. Lengo ni kujiridhisha kama utaratibu wa kiserikali umefuatwa.

### **D. Tozo/Malipo**

Kibali cha kuingiza chakula cha samaki katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi mpaka sasa hakilipiwi. Aidha chakula cha samaki kwa sasa kimepewa msamaha wakodi.

### **E. Ushauri wa kuzingatia**

- ✓ Muagizaji wa chakula cha samaki anapaswa kuwa na ghala la kuhifadhia chakula cha samaki kwa ajili ya kuhakikisha usalama na ubora wa chakula hicho.
- ✓ Kibali cha kuingiza chakula cha samaki nchini hakihamishiki na kinatolewa kwa kiasi kilichoombewa tu kwa muda maalum.
- ✓ Hairuhusiwi chakula cha samaki kiwe na madawa hatarishi, viutilifu au dawa yeyote itakayochochea ukuaji wa samaki
- ✓ Chakula cha samaki kiagizwe kutoka kwenye viwanda vyenye ithibati ya ubora.